

Ijapokuwa *Safflower* pekee ina faida nyingi, ni vyema kukuza pamoja na mimea mingine ya kitamaduni.

### **Wadudu na Magonjwa**

Magonjwa kadhaa yanayosababishwa na ukungu pamoja na bakteria huvamia *Safflower*. Kupanda mbegu safi bila magonjwa, kutibu mbegu na utumiaji wa kemikali ni moja kati ya mambo yanastahili kutekelezwa.

Kuathiriwa kunaweza kuenea katika mmea kutokana na masalio ya mmea ya awali, kwa hivyo ukuzaji wa mimea wa mzunguko unafaa kuzingatiwa vyema. Ukosefu wa maji huharakisha kuenea kwa magonjwa na kwa hivyo uchaguzi wa shamba ni muhimu sana.

### **Uchunaji, Kukausha na kusaga**

Aina nyingi hukomaa kwa muda wa siku 115-140.

- Chuna wakati majani yake yamekauka na kuwa ya hudhurungi.
- Kata asubuhi mapema wakati miiba yake ni laini.
- Ipange shambani hadi ikanke vizuri. Weka katika kifagio kinachoendeshwa au saga kwa vijiti kisha upulize kwenye upepo.



### **Kenya Agricultural Research Institute**

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Barua pepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

#### **Mtayarishaji:**

Mahasi, J.M.

#### **Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:**

#### **Mkurugenzi wa Kituo,**

KARI- Lanet

S.L.P. Njoro,

Simu: 0203510-865

Barua pepe: karinjoro@karinjoro.org

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 54 /2008


**Shilingi 20 za Kenya**

## **Ukuzaji wa mmea wa *Safflower* katika sehemu kavu nchini Kenya**



## Utangulizi

*Safflower* ni mmea wenye mizizi yenye kimo, inayoweza kuhimili kiangazi. Huu mmea una mbegu zenye mafuta.




Mmea wa *Safflower*

Shina lake limegawanyika kati ya sehemu 1 hadi 5 zenye maua kwa kila tawi. Kila moja lina mbegu 15 hadi 20. Aghalabu, maua ni ya rangi ya majano, mekundu au meupe. Aina zote, zenye miiba au zile hazina, zaweza kukua Kenya.

## Umuhimu wa kiuchumi

*Safflower* ni chanzo cha viposho vyenye mafuta ya kuliwa, chakula cha mifugo na mafuta ya kutumika katika kampuni. Bei yake ni ya juu kote duniani kwa kuwa ni muhimu na salama kwa mazingira. Mafuta yake yameonekana ni muhimu kupunguza kolesteroli ya damu na kuponya magonjwa mengi yanayowadhuru wanawake.

Umuhimu zaidi ni kuboresha muundo wa mchanga kuzuia magonjwa, kutumika kutengeneza



Msitu wa *Safflower*

vitu vya mapambo, mboga na vyakula vya mifugo. Umuhimu zaidi ni kuboresha muundo wa mchanga kuzuia magonjwa, kutumika kutengeneza bidhaa za mapambo, mboga na vyakula vya mifugo.

## Hali ya kukuza

Mvua: kiwango cha milimita 250-650.

Mchanga: Mchanga uliyona rutuba, ya kimo, unaoteremsha maji vyema na wenye kiwango cha kati cha unyevu. Aidha unaohifadhi maji kwa kiwango kinachofaa.

Mizizi yenye kimo inasaidia kutumia maji na virutubishi kutoka chini ya sehemu ya mizizi. Ina uwezo wa kufanya vizuri katika mchanga uliyo na chumvi.

Kiangazi: Mmea huu unaweza kuhimili kiangazi kwa kupunguza kiwango cha muda wa kukomaa ili kutumia maji yaliyoko mchangani.

## Sehemu za ukuzaji

Sehemu kavu kama vile Marsabit, Naivasha na Gilgil miongoni mwa zingine.

## Matayarisho ya Kitalu

*Safflower* inahitaji shamba la mbegu lenye mchanga thabiti na nyevunyevu kwa kiwango kinachofaa kwa maandalizi bora. Kulima kunafaa kuzuia kiwango cha juu cha maji kwenye uchanga ili kupatikana kwa kitalu mwafaka.

## Mahitaji ya mbolea na samadi

Samadi ya shambani au kinyesi cha mifugo tani 5 kwa kila ekari zinazofaa kuchanganywa na mchanga wakati wa matayarisho ya shamba ili kuimarisha uwezekano wa mchanga kuhifadhi maji na kuipa mimea virutubishi kwa mazao ya juu. Kilo 5 kwa kila ekari ya P na kilo 50 kwa kila ekari ya nitrojeni sharti kutumiwa.

## Kupanda

Wakati wa kupanda sharti ulingane na mwanzo wa mvua.

- Katika Mihimili maalum, tumia kilo 10-12 za mbegu zilizo kati ya sentimita 45x20.
- Katika hali ya maji kidogo kwa mchanga, tumbukiza mbegu majini kwa muda wa masaa 24 hadi 48 tena ukaushe chini ya kivuli kwa muda wa saa nne. Tibu kwa kutumia dawa za ukungu kabla ya kupanda.